# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU - KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU, MH. PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB), KATIKA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI - MOROGORO, 28 APRILI 2023

- Mhe. Patrobas Paschal Katambi (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu),

- Prof. Jamal Adam Katundu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu),

- Mhe. Fatma Abubakar Mwassa, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro,

- Dr. Mussa Ali Mussa, Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro

- Ndugu Rebeca Sanga Msemwa, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro

- Bi. Khadija Mwenda, Mtendaji Mkuu Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA),

- Bi. Suzanne Ndomba-Doran, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE),
- Ndugu. Tumain Nyamhokya,Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),
- Ndugu. Henry Mkunda, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA),
- Ndugu Wellington Chibebe, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa nchi za Tanzania, Burundi, Kenya, Rwanda and Uganda,
- Viongozi na Wafanyakazi wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi Zake,
- Ndgu Wandishi wa Habari
- Wageni Waalikwa,
- Mabibi na Mabwana

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Awali ya yote ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani, kwa lengo la kuhamasisha waajiri, wafanyakazi na umma kwa ujumla ili waweze kuweka mikakati ya kupunguza kama sio kuzuia kabisa magojwa na ajali zinazotokea kazini.

Kipekee Niishukuru sana Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho haya iliyokuwa ikiongozwa na Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bibi **Khadija Mwenda** kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi katika siku hii muhimu ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani. **Asante sana.**

Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Uongozi wa Mkoa wa Morogoro hususan Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. **Fatma Abubakar Mwassa**, kwa kukubali kuwa mwenyeji wetu katika maadhimisho ya siku hii. Kwa kweli ametupatia ushirikiano wa hali ya juu lakini pia kwa mapokezi mazuri ambayo nimeyapata toka nilivyofika Mkoani Morogoro.

Pia ninawapongeza Viongozi wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Wadau wengine ambao kwa namna moja ama nyingine wamefanya kazi kwa bidii na kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha kuwa siku hii ya leo inafanikiwa. **Hongereni sana**

Nimefurahi sana kuona wadau wengi wa Masuala ya usalama na afya mahali pa kazi, ambao wamekuja kwenye maonesho na kutoa huduma mbalimbali kwenye maadhimisho haya. **Asanteni sana**

Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro hasa Wafanyakazi kwa kujitokeza kwa wingi katika siku hii muhimu ambapo Tanzania inaungana na Jumuiya za Kimataifa kuadhimisha siku ya Usalama na Afya mahali pa Kazi Duniani.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Nimepewa taarifa kwamba, kuelekea Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Usalama Mahala Pazi Duniani, kwa mwaka 2023, kumekuwa na shughuli mbalimbali ambazo zimeratibiwa na OSHA ikiwa pamoja na kufanya Kaguzi na Upimaji wa mazingira na Afya kwa wafanyakazi wa Vyombo vya habari vya TBC, Wasafi TV, EFM, Uhuru FM, na Channel Ten. Aidha, katika kuhakikisha kunajengwa utamaduni wa kujikinga na majanga mbalimbali nimeambiwa kumetolewa Mafunzo ya Usalama na Afya kwa wanafunzi takribani **559** wa Vyuo mbalimbali nchini kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),

Chuo cha Maji, Chuo cha Usafirishaji (NIT) na Chuo Kikuu cha Muhimbili.

Nimepewa taarifa pia yametolewa Mafunzo ya Usalama na Afya mahala pa Kazi kwa wafanyakazi wa viwandani na wajasiliamali katika Mikoa ya Morogoro, Lindi, Mtwara, Geita, Dar es Salaam na Pwani ambapo takribani ya Wafanyakazi **4,000** wamefikiwa.

Aidha, katika kuadhimisha siku hii, yametolewa pia Mafunzo ya Usalama na Afya kwa vyombo mbalimbali vinavyosimamia Haki nchini ikiwa pamoja na Mawakili wa Serikali na Chama cha wanasheria (TLS) wapatao **200** ili wanapotekeleza majukumu yao wazingatie pia Masuala ya usalama na Afya.

Niwapongeze sana OSHA na Wadau kwa kuendelea kutekeleza wajibu huu muhimu kwa ustawi wa Wafanyakazi na Umma hapa nchini.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Kama tunavyofahamu chimbuko la siku hii ilikuwa ni harakati za Chama cha Wafanyakazi Duniani katika kuwakumbuka wafanyakazi waliopoteza maisha, kupata ulemavu ama kupata magonjwa yatokanayo na kazi wakati wakitekeleza majukumu yao sehemu za kazi ambayo ilianzia huko New York, Marekani mwaka wa 1996.

Napenda kuchukua furusa hii kutoa pongezi maalum na za dhati kwa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa uamuzi wao wa kuwaunga mkono Chama cha Wafanyakazi Duniani na kubadilisha maudhui ya siku hii. Badala ya kukusanyika na kuwasha mishumaa ya maombolezo ya wafanyakazi waliopoteza maisha, Shirika la Kazi Duniani waliona ni vema kuibadilisha siku hii ili iwe siku ya kuhamasisha na kuweka mikakati ya kulinda wafanyakazi ili wasiendelee kupoteza maisha wakiwa kazini.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Serikali yenu inayoongozwa na ***Dkt. Samia Suluhu Hassan*** inatambua kuwa Masuala ya Afya na Usalama mahala Pa Kazi ni haki ya Msingi kwa kila Mfanyakazi hapa nchini. Mheshimiwa Rais, amekuwa kinara wa kuhakikisha kuwa Nguvu Kazi ya Taifa inalindwa kwa kuendelea kuimarisha Taasisi ya OSHA. Kupitia Taasisi ya OSHA Serikali inaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa **Sheria Na. 5 ya Afya na Usalama mahala pa kazi ya mwaka 2003**, lengo ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ya Kazi Nchini yanakuwa na mifumo madhubuti ya kuwakinga wafanyakazi dhidi ya ajali na magonjwa yatakanayo na kazi.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Siku ya Usalama na Afya Duniani ni siku muhimu ya Kimataifa ambayo Nchi zote wanachama wa Shirika la Kazi Duniani ziliombwa kuadhimisha siku hii.

Kuanzia mwaka 2003 zaidi ya Nchi 110 Duniani kote zinaadhimisha siku hii kwa lengo la kuwawezesha wadau kupanua uelewa kuhusu ukubwa na madhara ya ajali na magojwa yatokanayo na kazi na kujenga uwezo wa Nchi hizo katika kuweka Sera na Mikakati ya kuzuia ajali na magonjwa kazini ili kufanya kazi zote ziwe za Staha.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Kama mnavyofahamu huu ni mwaka wa kumi na tisa tangu tulipoanza kuadhimisha siku hii hapa Nchini kwetu kuanzia mwaka 2004. Kila mwaka tumekuwa na kauli mbiu mbalimbali zinazolenga kuhamasisha Waajiri na Wafanyakazi kufanya juhudi za makusudi ili kuzuia magonjwa na ajali kazini. Na mwaka huu kauli mbiu ni "***Mazingira salama na yenye afya kazini ni kanuni na haki ya msingi mahali pa kazi (A safe and healthy working environment is a fundamental principle and right at work)"***

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Kama mnavyojua, kauli mbiu hii imetokana na kikao cha Mkutano wa Shirika la Kazi Duniani, ILO uliofanyika huko Geneva Nchini Uswisi Juni 2022. Moja ya maazimio ya Mkutano huo ilikuwa ni kujumuisha suala la mazingira salama na yenye afya mahali pa kazi kama mojawapo ya kanuni na haki tano za kimsingi kazini.

Katika maamuzi hayo mikataba ya Usalama na Afya Kazini, **Na. 155** na Uendelezaji wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, **Na. 187** ilitangazwa kuwa mikataba ya msingi. Kutokana na uamuzi huo, Nchi zote Wanachama wa ILO, hata kama hazijaridhia Mikataba hiyo, zina wajibu wa kuheshimu, kukuza na kutambua kwa nia njema kwa mujibu wa Katiba ya ILO, kanuni zinazohusu haki za msingi ambazo ndizo agenda ya Mikataba hiyo.

Kwa mantiki hiyo Nchi yetu kama zilivyo Nchi nyingine tunaheshimu uamuzi huo na ni makusudio yetu kutekeleza matakwa ya vipengele vilivyomo kwenye mikataba hiyo hata kama hatujairidhia. Kwa hiyo sisi kama Serikali na kama alivyosema Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Hotuba yake ya Mei Mosi mwaka 2022 Jijini Dodoma, kwamba tupo katika hatua mbali mbali za kuridhia Mkataba Na. 155, tutahakikisha kuwa mchakato wa kuridhia mkataba Na. 187 nao unaanza na hatimae kufikishwa Bungeni mikataba yote miwili kwa kuwa ndiyo itakayowawezesha Wafanyakazi kupata haki yao ya msingi wakiwa kazini.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Moja ya majukumu ya Ofisi yangu ni kulinda Usalama na Afya wa Wafanyakazi wanapokua maeneo ya kazi. Usalama na Afya mahali pa kazi ni moja kati ya masuala ya kazi kama ilivyo masuala mengine ya wafanyakazi.

Ikiwa suala la usalama na afya mahali pa kazi halitazingatiwa kuna athari nyingi ikiwa pamoja na upotevu wa maisha ya wafanyakazi na pia kuathiri utendaji wa kazi wakati wafanyakazi waliomia wakiendelea kupata matibabu. Kwa maana hiyo ningependa kuchukua fursa hii kuwataka Waajiri wote Nchini wachukue hatua ya kuhakikisha kwamba wanalinda usalama na afya za wafanyakazi wao kama yalivyo matakwa ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi Namba 5 ya mwaka 2003.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Upo ukweli kwamba magojwa, ajali na vifo vinavyotokea sehemu za kazi vinaweza kuzuilika kwani dalili za kutokea kwake zinaanza kuonekana mapema. Ili kuzuia magonjwa, ajali na vifo inatakiwa kuweka mifumo sahihi ya usalama na afya mahali pa kazi na kuzingatia sheria na kanuni za Usalama na Afya sehemu za kazi.

Mifumo hiyo inatakiwa kuzingatia vihatarishi vya dharura na utayari wa kukabiliana na magojwa ya mlipuko kama vile ilivyotokea wakati wa UVIKO-19. Kwa bahati mbaya waajiri wengi hawajaweka hiyo mifumo na wengine hawana ufahamu wa namna ya kuweka mifumo hiyo, hivyo nawasisitiza Waajiri wote washirikiane na OSHA ili kuhakikisha mifumo hiyo inawekwa maeneo ya Kazi.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Ndugu Wafanyakazi na Waajiri suala la janga la VVU na UKIMWI bado ni agenda kubwa Duniani pia ni moja kati ya vihatarishi vikubwa katika ulimwengu wa kazi kwa kuwa idadi kuwa ya Wafanyakazi ndio walioko kwenye umri hatarishi wa kuambukizwa ugonjwa huu.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2021 watu takribani milioni 40.1 walikuwa wamepoteza maisha Duniani kote kwa sababu ya VVU na UKIMWI.

Takwimu hizo pia zinaonyesha kuwa takribani watu **milioni 38.4** wanaishi na virusi vya UKIMWI na kati ya hao **milioni 25.6** wapo katika Bara la Afrika.

Katika Utafiti wa Viashiria na Matokea ya UKIMWI Tanzania ya mwaka 2016/17, ulionyesha kuwa kiwango cha maambukizi ya VVU kwa watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 Nchini ni asilimia 5.0 na maambukizi mapya ni asilimia 0.25. Pamoja na kupungua kwa maambukizi ya UKIMWI Nchini na Duniani lakini bado takwimu hizo kimsingi sio za kupuuza.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Napenda kuwakumbusha kwamba bado dawa ya kutibu ugojwa wa UKIMWI haijapatikana. Hivyo katika kupambana na hili janga la UKIMWI, mapambano ni lazima yalenge katika kutatua matatizo yanayokwamisha mapambano ya UKIMWI.

Matatizo hayo ni ufahamu mdogo kuhusu UKIMWI, waathirika kutojitokeza na kuwa wawazi kwa watu waliokaribu nao, unyanyapaa, ngono zembe, rushwa ya ngono sehemu za kazi, na kuwanyima haki waathirika wa UKIMWI.

Kwa hiyo tunapoungana na wenzetu Duniani kuadhimisha siku ya Usalama na Afya Kazini hatuna budi kuwakumbusha Waajiri na Wafanyakazi kwa pamoja kuweka mikakati inayolenga kuwashawishi wafanyakazi juu upimaji wa hiyari na ushauri nasaha, kuzuia maambukizi mapya sehemu za kazi, kuweka sera zinazolenga kuwasaidia wale wafanyakazi ambao tayari wameathirika, kupunguza unyanyapaa na kuwawezesha waathirika kupata matibabu ya magonjwa nyemelezi kila yanopojitokeza. Kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeiokoa nguvu kazi ambayo ndiyo inayotegemewa katika uzalisha mali na ukuaji wa uchumi na tija ya Taifa.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Sekta isiyo rasmi na sehemu ndogondogo za kazi zina mchango mkubwa katika uchumi wa Nchi yetu. Lakini kwa bahati mbaya wafanyakazi katika sekta hii wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Mara nyingi huduma ya ukaguzi wa afya na usalama kazini haiwafikii wafanyakazi katika sekta hii. Katika sekta hii viwango vya ajali na magojwa yatokanayo na kazi yawezekana vikawa vikubwa sana. Kwa bahati mbaya kwa sasa hakuna mfumo ulioandaliwa wa kuripoti ajali na magonjwa hayo unaofanya kazi kwa sasa katika sekta hii. Hali hiyo inasababisha kushidwa kufahamu kwa uhakika hali halisi ya usalama na afya katika sekta hiyo. Hivyo wakati tunaadhimisha Siku ya Afya na Usalama Mahala Pa kazi niwasisitize OSHA kwa kushirikiana na wadau wengine kuangalia uwezekano wa kufahamu hali halisi katika sekta hii ili tuangalie namna ya kuwasaidia Watanzania hawa wasiendelee kupata madhara wakiwa kazini.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Serikali yetu inathamini na kutambua juhudi za Taasisi za umma na binafsi zinazojituma katika kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wao bila kushurutishwa. Serikali kwa kupitia Wakala wa Usalama na Afya mahali pa Kazi (OSHA), imeanzisha tuzo kwa Taasisi zinazoonyesha juhudi katika kuboresha mazingira ya kazi. Napenda, nichukue furusa hii kuzipongeza Taasisi zitakazofanikiwa kupata hizo tuzo kwa mwaka huu. Leo zitatolewa Tuzo za aina mbali mbali kadri ilivyopangwa na nina imani kuwa kila mmoja wenu atapata Tuzo. Nichukue fursa hii kuwaasa wale watakaopata Tuzo kwamba wasibweteke na hizo Tuzo, bali waendelee kuimarisha usalama na afya kwa wafanyakazi wao.

***Ndugu Wafanyakazi na Waajiri,***

Nikielekea Kuhitimisha Hotuba yangu, sote tunafahamu kuwa zimesalia siku tatu tu tufikie kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei

Mosi 2023. Namna bora ya kuadhimisha siku ya Mei Mosi ni kwa Wafanyakazi kujitathmini kila mmoja ni kwa namna gani tumeweka juhudi za kujilinda na vihatarishi sisi wenyewe na wale tunaofanyakazi pamoja, na kwa kiasi gani tutashirikiana na Waajiri wetu katika kutengeneza mazingara ya kudumisha haki za msingi za wafanyakazi wakiwa kazini.

Niwasihi Wafanyakazi, Waajiri na Wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro na mikoa ya jirani kujitokeza kwa wingi katika siku ya kilele ya Mei Mosi ili tuweze kusherehekea siku hii kwa pamoja. Kwa wale watakaoweza kufika katika uwanja wa Mpira wa Miguu wa Jamhuri hapa mjini Morogoro siku ya tarehe 1 Mei,2023 karibuni sana.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Napenda nirudie kutoa pongezi zangu kwa Wafanyakazi na Wananchi wote wa mkoa wa Morogoro kwa kufanikisha maadhimisho ya Siku ya

Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani mwaka huu, na niwakumbushe tena “***Mazingira salama na yenye afya kazini ni kanuni na haki ya msingi mahali pa kazi***.

**Ndugu Waajiri, Wafanyakazi na Wadau;**

Mwisho ningependa kusisitiza kuwa, serikali itaendelea kusimamia suala la Usalama na Afya Mahala pa Kazi, hivyo tunawaomba wadau wetu muendelea kushirikiana na sisi ili kutimiza azima hii ambayo inalenga kupunguza au hata ikiwezekana kuondoa kabisa vifo, ajali, magonjwa na madhara yatokanayo na kazi. Kwa pamoja kama Taifa tutaweza kupata suluhisho la matatizo ya usalama na afya yanayowapata wafanyakazi wakiwa kazini.

Baada ya kusema hayo kwa mara nyingine napenda kuwashukuru wote mlioshiriki kikamilifu katika maadhimisho haya na ninawatakia siku njema.

**Asante kwa kunisikiliza.**